



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI  
ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA USHETU



Unapojibu tafadhali taja:  
Kumb. Na. UDC/L.40/8/47

01 Novemba 2023

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA MKATABA**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu anawatangazia nafasi za kazi watanzania wote wenye sifa za kuajiriwa kwa mkataba katika nafasi ya Dereva Daraja la II.

**1. Dereva Daraja II – NAFASI 4**

**A. Sifa za Mwombaji**

1. Awe amehitimu Kidato cha Nne (IV)
2. Awe mwenye leseni ya daraja C ya kuendelea Magari
3. Mwenye uzoefu wa kuendesha magari kwa muda usiopungua miaka mitatu (3) bila kusababisha ajari.

NB: Mwenye cheti cha Majaribio ya Ufundi Daraja la II (Trade Test Level II) atapewa kipaumbele.

**B. Kazi/Majukumu**

1. Kuendesha magari ya abiria, malori.
2. Kufanya matengenezo madogo madogo katika gari.
3. Kutunza na kuandika daftari la safari "Log book" kwa safari zote.
4. Kuhakikisha gari na vyombo vyake vipo katika hali nzuri wakati wote na kufanya uchunguzi wa gari kabla, na baada ya safari ili kugundua ubovu unaohitaji matengenezo.

**C. Mshahara: Ngazi ya Mshahara wa Serikali (TGS B)**

**D. Vigezo na Masharti ya Jumla kwa waombaji.**

1. Mwombaji awe raia wa Tanzania na umri usiozidi miaka 45 na usiopungua miaka 18
2. Mwombaji awe hajawahi kushitakiwa kwa kosa lolote la jinai.
3. Mwombaji aambatanishe nakala za vyeti vya taaluma, nakala ya cheti cha kidato cha nne vilivyothibitishwa na Hakimu au Wakili anayetambulika na Serikali.

4. Mwombaji aambatanishe nakala ya Leseni Daraja C ya uendeshaji magari iliyothibitishwa na Hakimu au Wakili anayetambulika na Serikali.
5. Waombaji wote waambatanishe nakala ya cheti cha kuzaliwa kilichothibitishwa na Hakimu au Wakili anayetambulika na Serikali.
6. Waombaji wote waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed Curriculum Vitae) ikiwa na anuani, namba za simu za kuaminika, pamoja na majina ya wadhamini (Referees) watatu (3) na picha mbili za "passport size" za hivi karibuni (ziandikwe jina kwa nyuma).
7. Testimonials, provisional results, Statement of results na hati za matokeo ya kidato cha nne na sita (form IV na form VI) result slips HAITAKUBALIWA.
8. Mwombaji aliyesoma elimu ya kidato cha nne (4) nje ya Tanzania ahakikishe vyeti vyao vimekaguliwa na kuthibitis
9. hwa na Mamlaka husika (NECTA au NACTE).
10. Mwombaji aliyestaafu katika Utumishi wa Umma haruhusiwi kuomba isipokuwa kama na kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
11. Waombaji watakaowasilisha vyeti, na taarifa za kughushi watachukuliwa hatua za kisheria na mamlaka zinazohusika.
12. Maombi yote yaandikwe kwa mkono na kwa lugha ya Kiswahili.
13. Waombaji wote waambatanishe Namba ya Utambulisho wa Uraia (National Identification Numbe) kutoka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA). Utambulisho huo uwe umethibitishwa na Afisa Usajili Wilaya, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).
14. Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni siku ya Jumanne, tarehe 14 Novemba 2023, saa 09:30 Alasiri.
15. Maombi yote yatumwe kwa njia ya posta kupitia anuani ifuatayo;

Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu,  
S. L. P 50,  
**KAHAMA.**

  
Hadija M. Kabojela  
MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
USHETU



**NAKALA:** Katibu Tawala (M),  
S. L. P 320,  
**SHINYANGA.**

Katibu Tawala (W),  
S.L.P 01,  
**KAHAMA.**

Mbao zote za Matangazo,  
Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu, Msalala na Manispaa ya Kahama.  
**KAHAMA.**